



# Bima ya Child Health Plus kwa Ufupi

## NI NANI ANAYESTAHIKI?

### WATOTO AMBAO:

- Wana umri wa chini ya miaka 19
- Ni wakazi wa Jimbo la New York
- Hawastahiki kupokea bima ya Medicaid
- Hawana bima nyingine ya afya
- Hawastahiki au hawajasajiliwa katika bima ya afya kupitia mpango wa huduma ya afya ya jimbo (NYSHIP)
- Watoto wanaweza kustahiki bila kuzingatia hali yao ya uhamiaji

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsia umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

## NINI HULIPIWA NA BIMA?

- Ziara za uchunguzi
- Uchunguzi wa kimwili
- Chanjo
- Huduma ya wagonjwa wanaolazwa
- Huduma za maabara na picha za tiba
- Huduma za Meno na Macho
- Huduma za dharura
- Tiba ya muda mfupi ya kimwili na kikazi.
- Dawu zisizo za kuagizwa na daktari, ikiwa utaruhusiwa na daktari
- Huduma za wagonjwa wasiolala za tiba za muda mfupi (tibakemo, usafishaji wa damu)
- Huduma za afya ya kiakili na ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevyu kulevyu kwa wagonjwa wanaolazwa na wasiolazwa
- Huduma za Kuongea na Kusikia

Hii si orodha kamili ya mafao yanayolipwa na bima. Unapaswa kuwasiliana na bima yako ya afya moja kwa moja kwa maswali yoyote kuhusu huduma na mafao yanayolipwa kupitia mpango wako wa afya na watoa huduma.

### WASILIANA NASI:

[nystateofhealth.ny.gov](http://nystateofhealth.ny.gov) | 1-855-355-5777 au TTY 1-800-662-1220

# GHARAMA YA MPANGO WA CHILD HEALTH PLUS NI GANI?

**MALIPO YA KILA MWEZI:** Bei ya kila mwezi hutegemeana na pato la familia na ukubwa wa familia.\* Hakuna malipo ya juu ya kila mwezi kwa familia zenye mapato ya chini. Familia zenye mapato ya juu hulipa malipo ya juu ya kila mwezi, kulinga na jedwali hapa chini. Kwa familia kubwa zaidi, kiwango cha juu zaidi cha ada ya kila mwezi ni cha watoto watatu tu. Familia zenye mapato ya kiasi cha juu ya kilichojumuishwa kwenye bima wanaweza kulipa kiasi chote, kinachotofautiana kulingana na mpango mahususi wa afya.

**KUGAWANA GHARAMA:** Mpango wa Child Health Plus hauna ada za kila mwaka zinazokatwa wala malipo saidizi.

Kiasi cha Juu Zaidi cha Mapato ya Kila Mwaka Kulingana na Ukubwa ywa Familia				Mchango wa Kila Mwezi kwa Kila Mtoto (idadi ya juu zaidi ya watoto unaolipia ni 3)
1	2	3	4	
\$32,368	\$43,779	\$55,190	\$66,600	\$0
\$36,450	\$49,300	\$62,150	\$75,000	\$15 (kiasi cha juu zaidi cha \$45)
\$43,740	\$59,160	\$74,580	\$90,000	\$30 (kiasi cha juu zaidi cha \$90)
\$51,030	\$69,020	\$87,010	\$105,000	\$45 (kiasi cha juu zaidi cha \$135)
\$58,320	\$78,880	\$99,440	\$120,000	\$60 (kiasi cha juu zaidi cha \$180)
zaidi ya \$58,320	zaidi ya \$78,880	zaidi ya \$99,440	zaidi ya \$120,000	Malipo kamili ya bima yanatofautiana kulingana na mpango wa afya (hakuna kiasi cha juu zaidi cha familia)

\*Kulingana na Viwango vya Mali vya Shirikisho (FPL) 2023 Viwango vya mapato vinaweza kurekebishwa kila mwaka kulingana na mabadiliko ya FPL.